**SERIKALI YA MAPINDUZI ZANZIBAR**

**WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO**

# HOTUBA YA WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO

**MHESHIMIWA RIZIKI PEMBE JUMA (MBM)**

**KATIKA BARAZA LA WAWAKILISHI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025**

**JUNI, 2024**



**Mhe. Riziki Pembe Juma (MBM)**
**Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia,Wazee na Watoto**



**Mhe. Anna Athanas Paul**
**Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia,Wazee na Watoto**



**Ndg. Abeida Rashid Abdallah**
**Katibu Mkuu Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia,Wazee na Watoto**



**Ndg. Khatib Mwadini Khatib**
**Naibu Katibu MkuuWizara ya Maendeleo**
**ya Jamii, Jinsia,Wazee na Watoto**



**Ndg. Hafidh Ali Mohamed**
**Afisa Mdhamini Wizara ya Maendeleo**
**ya Jamii, Jinsia,Wazee na Watoto**



**Dkt. Salum Khamis Rashid**
**Mkurugenzi Utumishi na**
**Uendeshaji**
**Wizara ya Maendeleo**
**ya Jamii, Jinsia,Wazee na Watoto**



**Ndg. Daima Mohamed Mkalimoto**
**Mkurugenzi Mipango, Sera na**
**Utafiti**
**Wizara ya Maendeleo**
**ya Jamii, Jinsia,Wazee na Watoto**



**Ndg. Hassan Ibrahim Suleiman**
**Mkurugenzi Ustawi wa Jamii**
**Wizara ya Maendeleo**
**ya Jamii, Jinsia,Wazee na Watoto**



**Ndg. Siti Abbas Ali**
**Mkurugenzi Maendeleo ya Jamii**
**Jinsia na Watoto**
**Wizara ya Maendeleo**
**ya Jamii, Jinsia,Wazee na Watoto**



**Ndg. Shaame Ali Ali**
**Mhasibu Mkuu**
**Wizara ya Maendeleo**
**ya Jamii, Jinsia,Wazee na Watoto**

## YALIYOMO


VIFUPISHIO VYA MANENO .................................... vii
A. UTANGULIZI.......................................................... 1
B. MUUNDO NA MAJUKUMU YA WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO ............................................................... 4
C. UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA KWA KIPINDI CHA JULAI 2023 – MACHI 2024 ... 5
*Mapato na Matumizi* .................................................. *5*
*Mafanikio na Changamoto* ......................................... *7*
D.UTEKELEZAJI WA MIRADI INAYOSIMAMIWA NA WIZARA ....................................................... 10
E. UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA PROGRAMU ZA FUNGU LA WIZARA..................................11
*Programu ya Hifadhi ya Jamii*................................. *12*
*Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara*....... *17*
*Programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji* ........... *18*
*Programu ndogo ya Uratibu Mipango, Sera na Utafiti* ...................................................................... *20*
*Programu ndogo ya Uratibu wa Wizara Pemba*........ *23*
*Programu ya Maendeleo ya Jamii na Jinsia* ............ *24*

F.MWELEKEO WA BAJETI YA WIZARA KWA MWAKA 2024/2025 ............................................... 32
*Programu ya Hifadhi ya Jamii (PH0401)*.................. *34*
*Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara (PH0402)*................................................................. *35*
*Programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji* ........... *35*

*Programu ndogo ya Uratibu wa Mipango, Sera na Utafiti* ........................................................................ *35*
*Programu ndogo ya Uratibu wa shughuli za Wizara Pemba* ...................................................................... *36*
*Programu ya Maendeleo ya Jamii na Jinsia* ............. *36*

G. SHUKRANI ........................................................ 37

H. HITIMISHO ........................................................ 41

# VIAMBATANISHO


Kiambatanisho Nam. 1: Muhtasari wa Upatikanaji wa Fedha kwa Kipindi cha Julai, 2023 - Machi 2024 .................. 45

Kiambatanisho Nam. 2: Makaazi ya Wazee Unguja na Pemba..................................... 46

Kiambatanisho Nam. 3: Taarifa ya Wazee walio katika Mpango wa Pencheni Jamii .... 46

Kiambatanisho Nam. 4: Malalamiko ya Matunzo na Mvutano wa Malezi ................ 47

Kiambatanisho nam. 5: Wahanga waliopo nyumba salama ..................................... 48

Kiambatanisho Nam. 6: Makosa yaliyopelekea watoto kupokelewa katika Kituo cha Marekebisho ya Tabia ............. 49

Kiambatanisho Nam. 7: Vituo Vya Kulelea Watoto Yatima ................................................ 49

Kiambatanisho Nam.8: Vituo vya Malezi na Makuzi ya . Awali ya Mtoto........................ 50

Kiambatanisho Nam.9a: Watumishi waliopo masomoni kwa muda Mrefu..................... 52

Kiambatanisho Nam.9b: Watumishi waliopo masomoni . kwa muda Mfupi..................... 53

Kiambatanisho Nam. 10: Idadi ya wafanyakazi kwa mujibu wa Elimu zao.......................... 54

Kiambatanisho nam. 11: Watendaji wa Wizara za SMZ .. waliopatiwa mafunzo ya Bajeti zenye kuzingatia Usawa wa Kijinsia .................................. 55

Kiambatanisho namba 12: Orodha ya vikundi vilivyotembelewa katika uhamasishaji wa uanzishaji wa Majukwaa ya Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi ............ 56

Kiambatisho nam. 13: Malalamiko ya Wanawake yaliyopokelewa ..................... 59

Kiambatisho nambari 14: Idadi ya vipindi vilivyorushwa vya Kupinga udhalilishaji kwa wanawake na watoto ..... 60

Kiambatanisho nam. 15: Mgawanyo wa fedha kwa mwaka wa fedha 2024/2025 . 61

# VIFUPISHIO VYA MANENO

| | |
|---|---|
| BAKIZA | Baraza la Kiswahili Zanzibar |
| CCM | Chama Cha Mapinduzi |
| CDC | Shirika la Afya ya Jamii |
| CRDB | Benki ya Biashara Tanzania |
| CRF | Shirika la Mtandao wa Haki za Watoto Zanzibar |
| C-SEMA | Huduma ya Simu ya Mtoto |
| DPP | Mkurugenzi wa Mashtaka |
| EU | Umoja wa Nchi za Ulaya |
| GEF | Jukwaa la Kizazi chenye Usawa |
| IOM | Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshu ghulikia Wahamiaji |
| IPA | Chuo cha Utawala wa Umma |
| ITV | Independent Television |
| JKU | Jeshi la Kujenga Uchumi |
| JUWAZA | Jumuiya ya Wastaafu na Wazee Zanzibar |
| JUYAWAZA | Jumuiya ya Wazee Zanzibar |
| KIU | Kampala International University |
| LSF | Huduma wa Msaada wa Kisheria |
| NBS | Ofisi ya Taifa ya Takwimu |
| NMB | Benki ya Taifa ya Biashara Ndogo ndogo |
| NPA-VAWC | Mpango wa Taifa wa Kupinga Ukatili na Udhalilishaji wa Wanawake na Watoto |

| | |
|---|---|
| PBB | Mfumo wa Bajeti unaozingatia Programu |
| PBZ | Benki ya Watu wa Zanzibar |
| PhD | Shahada ya Uzamivu |
| SMT | Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania |
| SMZ | Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar |
| SUZA | Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar |
| TAMWA | Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania |
| TBC | Shirika la Habari Tanzania |
| THESODE | Theatre for Social Development |
| THPS | Tanzania Health Promotion Support |
| TIRA | Mamlaka ya Bima Tanzania |
| TRA | Mamlaka ya Mapato Tanzania |
| UAE | Umoja wa Falme za Kiarabu |
| UNFPA | Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Idadi ya Watu |
| UNICEF | Shirika la Umoja wa Mataifa Watoto |
| UNWOMEN | Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia masuala ya Wanawake |
| USAID | Shirika la Misaada la Marekani |
| UWT | Umoja wa Wanawake Tanzania |
| WHO | Shirika la Afya Duniani |
| ZACA | Jumuiya ya Misaada ya Watoto |
| ZAECA | Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi |

| | |
|---|---|
| ZAFELA | Jumuiya ya Wanasheria Wanawake Zanzibar |
| ZAMWASO | Jumuiya ya Misaada ya Wanawake wa Kiislamu |
| ZAPHA+ | Jumuiya ya Watu Wanaoishi na Virusi vya UKIMWI |
| ZASO | Jumuiya ya Kusaidia Watoto Yatima na Wanaishi na Virusi vya UKIMWI |
| ZASWA | Jumuiya ya Maafisa ustawi wa jamii Zanzibar |
| ZBC | Shirika la Utangazaji Zanzibar |
| ZC TV | Zanzibar Cable Television |
| ZPC | Shirika la Bandari Zanzibar |
| ZSSF | Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar |
| ZSTC | Shirika la Biashara la Taifa Zanzibar |
| ZURA | Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar |
| ZU | Chuo Kikuu cha Zanzibar |

## A. UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika,** kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha hotuba ya bajeti kwa ajili ya kujadili na hatimaye kuiidhinishia Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto bajeti kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

2. **Mheshimiwa Spika,** kwanza kabisa naomba kutumia fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kutujaalia uhai, uzima na afya na kutuwezesha kukutana kujadili bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

3. **Mheshimiwa Spika,** natoa shukurani za pekee kwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, **Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi** kwa kuiongoza nchi yetu ikiwa na amani na utulivu pamoja na juhudi kubwa anazozichukua katika kuhakikisha jamii ya Wazanzibari inakuwa na ustawi na maendeleo endelevu kupitia uongozi wake wa busara na hekima. Aidha, Wizara inapenda kutoa shukurani za dhati kwa Mheshimiwa Rais kwa kuongeza kiwango cha Pencheni Jamii kutoka shilingi 20,000.00 hadi shilingi 50,000.00 sawa na ongezeko la asilimia 150 kuanzia Julai 2023. Ongezeko hili linaonesha mapenzi ya dhati ya **Mheshimiwa Rais** kwa wazee wetu ikiwa ni kutambua na kuthamini michango yao kwa taifa. Aidha, nachukua

fursa hii pia kuungana na watanzania wote kutoa pole kwa mara nyingine tena kwa Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi **Dkt. Hussein Ali Mwinyi** pamoja na familia yake, kufuatia msiba wa Mzee wetu Rais Mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Marehemu Mzee Ali Hassan Mwinyi. Tunamuomba Mwenyezi Mungu ampe malazi mema peponi, Amin.

4. **Mheshimiwa Spika,** kipekee naomba kutumia fursa hii kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, **Mheshimwa Dkt. Samia Suluhu Hassan** kwa juhudi anazozichukua katika kuleta usawa wa kijinsia na maendeleo kwa ujumla. Uongozi wake umeweza kusimamia umoja na mshikamano hadi sasa imetimiza miaka 60 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar tukiwa tumeshikamana kwa upendo na tumeimarika.

5. **Mheshimiwa Spika,** shukurani za dhati ziende kwa Makamu wa Kwanza wa Rais **Mheshimiwa Othman Masoud Othman** na Makamu wa Pili wa Rais **Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdullah** kwa kumsaidia na kumshauri vyema Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi katika utekelezaji wa majukumu ya Serikali Mapinduzi Zanzibar kutoa huduma bora kwa wananchi na za kimaendeleo.

6. **Mheshimiwa Spika,** kwa moyo wa dhati kabisa naomba kuchukua fursa hii kumpongeza mama yetu mpendwa, mke wa Rais wa Zanzibar, na Mwenyekiti wa Jumuiya ya Zanzibar Maisha Bora **Mama Mariam Mwinyi**, kwa kuwa sambamba na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto katika kusaidia maendeleo ya wanawake, watoto, wazee na ustawi wa jamii kwa ujumla.

7. **Mheshimiwa Spika,** naomba nikupongeze wewe binafsi Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wenyeviti wa Baraza lako tukufu pamoja na Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati mbali mbali za Baraza kwa kufanya kazi zao kwa umakini na uweledi. Uongozi wenu unaendelea kuwa wenye hekima na busara katika uendeshaji na usimamizi wa majukumu ya Baraza hili.

8. **Mheshimiwa Spika,** Wizara inatambua na kuthamini mchango mkubwa wa Kamati ya Ustawi wa Jamii ya Baraza la Wawakilishi inayoongozwa na Mwenyekiti wake **Mheshimiwa Sabiha Filfil Thani** na Makamu Mwenyekiti wake Mheshimiwa **Nassor Salim Ali** (Jazira) pamoja na Waheshimiwa Wajumbe na Makatibu wa Kamati kwa namna wanavyoshirikiana nasi katika kutekeleza majukumu yao kwa Wizara yangu, pia nashukuru sana kwa kuyapitia mapendekezo ya bajeti ya mwaka wa fedha 2024/2025 na kutoa michango ambayo imetuwezesha kuandaa hotuba hii na kuiwasilisha mbele ya Baraza hili tukufu.

## B. MUUNDO NA MAJUKUMU YA WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO

9. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto katika utekelezaji wa shughuli zake za kawaida zinatekelezwa kupitia Idara nne na Ofisi Kuu Pemba kama ifuatavyo:

   i. Idara ya Ustawi wa Jamii na Wazee;
   ii. Idara ya Uendeshaji na Utumishi;
   iii. Idara ya Mipango, Sera na Utafiti;
   iv. Idara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto; na
   v. Ofisi Kuu Pemba.

10. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto ina majukumu yafuatayo: -

   i. Kuweka mazingira bora ya Ustawi wa Jamii, Watoto, Wazee na kuratibu huduma ya Pencheni Jamii,
   ii. Kuimarisha hifadhi ya wazee na utoaji wa misaada ya kiustawi kwa wananchi wanaoishi katika mazingira magumu zaidi;
   iii. Kuandaa na kusimamia utekelezaji wa Sera, Mipango, Tafiti, Ufuatiliaji na Tathmini ya shughuli za Wizara;
   iv. Kusimamia maslahi ya rasilimali watu na nyenzo za utendaji kazi ikiwa ni pamoja na kuhifadhi na kutunza kumbukumbu;

v. Kuimarisha mfumo wa hifadhi ya mtoto na kusimamia haki na wajibu wao; na

vi. Kuimarisha uratibu wa ufikiwaji wa usawa wa kijinsia na kupambana na vitendo vya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia.

11. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kama zilivyo taasisi nyengine za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar inatumia mfumo wa bajeti unaozingatia programu (Program Based Budget - PBB) katika utekelezaji wa mpango kazi wake. Wizara imetekeleza shughuli zake kupitia programu kuu tatu ambazo ni:

i. Programu ya Hifadhi ya Jamii (PH0401)

ii. Programu ya Uratibu na Uendeshaji (PH0402) ambayo ina Programu ndogo zifuatazo: -

- Utawala na Uendeshaji (SH040201);
- Uratibu wa Sera, Mipango na Utafiti (SH040202);
- Utawala na Uendeshaji Ofisi Kuu Pemba (SH040203); na

iii. Programu ya Maendeleo ya Jamii na Jinsia (PH0403)

## C. UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA KWA KIPINDI CHA JULAI 2023 – MACHI 2024

### Mapato na Matumizi

12. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ilikadiriwa kukusanya kiasi cha shilingi 20,000,000.00 kwa mwaka wa fedha 2023/2024. Hadi kufikia Machi 2024, Wizara

imekusanya kiasi cha shilingi 5,200,000.00 sawa na asilimia 26 ya makisio ya mapato hayo na zimewasilishwa katika Mfuko Mkuu wa Serikali. Chanzo kikuu cha mapato haya ni Ukumbi wa Mikutano uliopo Sebleni ambapo kwa mwaka huu wa fedha Wizara inaufanyia matengenezo makubwa ili kuuimarisha sambamba na kufanyia matengenezo majengo mengine mawili.

13. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2023/24, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto ilikadiriwa kupata shilingi 9,887,311,000.00 zikiwemo fedha za matumizi ya kawaida shilingi 7,750,990,000.00 na za maendeleo ni shilingi 2,136,321,000.00. Kati ya fedha za kawaida zilizotengwa, shilingi 3,170,000,000.00 ni kwa ajili ya mishahara na shilingi 4,580,990,000.00 kwa matumizi mengineyo. Katika fedha za maendeleo zilizotengwa, shilingi 1,500,000,000.00 ni kutoka SMZ na shilingi 636,321,000.00 ni zamchango wa Washirika wa Maendeleo. Hadi kufikia mwezi Machi 2024, kwa upande wa matumizi ya kawaida fedha iliyopatikana ni shilingi 3,912,285,059.00 sawa na asilimia 50 ya makadirio ya mwaka. Kati ya fedha hizo shilingi 2,740,457,944.00 sawa na asilimia 86 ya fedha zilizopatikana zilitumika kwa ajili ya mishahara na shilingi 1,171,827,115.00 sawa na asilimia 26 zilitumika kwa ajili ya matumizi mengineyo. Aidha, kati ya matumizi hayo mengineyo shilingi 315,085,104.00 sawa na asilimia 54 ni fedha za mchango wa washirika wa Maendeleo. Kwa upande wa fedha za Maendeleo

fedha zilizopatikana ni shilingi 279,018,672.00 sawa na asilimia 13 ya makadirio ya mwaka. **Kiambatanisho nambari 1 kinatoa ufafanuzi.**

14. **Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa fedha iliyopatikana hadi Machi mwaka 2022/2023 ilikuwa ni shilingi 9,221,999,764 sawa na asilimia 58 ya makisio halisi. Fedha hiyo inahusisha pamoja na gharama za utekelezaji wa Mpango wa Pencheni Jamii. Kwa mwaka wa fedha 2023/2024 fedha iliyopatikana hadi kufikia Machi ilikuwa ni shilingi 4,506,388,835 sawa na asilimia 46.

**Mafanikio na Changamoto**

15. **Mheshimiwa Spika,** mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa mpango na bajeti ya Wizara ni kama ifuatavyo: -

    i. Kuongezeka kwa mashirikiano baina ya wanajamii na taasisi mbali mbali za ndani nan je pamoja na wadau wa maendeleo na ustawi wa jamii wakiwemo wanaopinga vitendo vya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia;
    ii. Kuendelea kuratibu mpango wa Pencheni Jamii ambapo mwaka 2023 kulikuwa na wazee 28,942 kwa sasa wamefikia wazee 30,127, sawa na ongezeko la wazee 1,185;
    iii. Uandaaji wa zana mbali mbali za uendeshaji wa Wizara ikiwemo Kanuni ya Vituo vya Malezi ya Kutwa (ECD), Mapitio ya Sheria ya Mtoto, Mapitio

ya Sera ya Mtoto, Muongozo wa uanzishaji na uendeshaji wa majukwaa ya uwezeshaji wanawake kiuchumi, zana ambazo ziko katika hatua za kukamilishwa;

iv. Wizara inaendelea kutoa msaada kwa watu wanaoishi katika mazingira magumu zaidi ambapo hadi Mwaka 2023, jumla ya familia 235 zilipokea msaada na hadi kufikia Machi 2024 idadi ya wanufaika imeongezeka na kufikia 283, sawa na ongezeko la familia 48.

v. Kuandaa na kuwasilisha ripoti mbili katika mikutano ya Umoja wa Mataifa New York, nchini Marekani ikiwemo ripoti ya Hali na Hadhi ya Wanawake (CSW68) na ripoti ya uwajibikaji katika utekelezaji wa Mpango wa Kizazi chenye Usawa (GEF);

vi. Kuwafikia wanawake kwa kuwapatia visaidizi vilivyoibua vipaji na ubunifu katika fani mbali mbali. Matokeo ya misaada hiyo iliamsha ari kwa wanawake kushindana katika kazi za maendeleo. Juhudi hizo zilifanyika kwa kushirikiana na Mwanamke Initiative Foundation.

vii. Kupatikana kwa utaalamu na ujuzi kwa wajasiriamali wanawake 50 na kuviunganisha vikundi 14 vya Wajasiriamali Wanawake kutoka katika Wilaya za Chake Chake, Mkoani, Wete na Micheweni kushiriki katika maonesho ya Siku ya Chakula Duniani; na

viii. Kuandaa na kuanza kutekeleza miradi ya maendeleo ikiwemo Mradi wa Maliza Vitendo vya Ukatili na Udhalilishaji kwa Wanawake na Wasichana (TOKOMEZA) na Mradi wa Kukuza Usawa wa Kijinsia (Advancing Gender Equality in Tanzania) unaotarajiwa kutekelezwa katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambapo Zanzibar ni sehemu ya mradi huo.

16. **Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha utekelezaji wa Julai 2023 hadi Machi 2024, Wizara imekabiliana na changamoto zifuatazo: -

i. Vitendo vya ukatili na udhalilishaji kwa wanawake na watoto kuendelea kujitokeza katika jamii ambapo Wizara inaendelea na zoezi la kutoa elimu kwa umma juu ya kukabiliana na vitendo hivyo;

ii. Kuwepo kwa wanawake wengi wenye uhitaji wa fursa za kiuchumi. Wizara inaendelea kuwahamasisha na kuwaelimisha wanawake jinsi ya kuimarisha uzalishaji na kuwaunganisha na taasisi za fedha na masoko;

iii. Ongezeka la idadi ya watoto wanaokinzana na sheria, ambapo mwaka 2023 kesi zilizofunguliwa ni 99 na mwaka 2024 zimefunguliwa kesi 365. Imepelekea Wizara kufanya mapitio ya Sheria ya Mtoto Nam. 6 ya mwaka 2011 na kuhamasisha jamii umuhimu wa malezi; na

iv. Uchakavu wa majengo ya Wazee Welezo, Limbani na Sebleni. Katika utatuzi wa hali hiyo, Wizara imeshafunga mkataba na mdau wa maendeleo Zayed bin Sultan Al Nahyan Charitable and Humanitarian Foundation kutoka nchini Qatar kujenga nyumba za kisasa za makaazi ya wazee Welezo. Aidha, kazi ya matengenezo ya majengo mawili na ukumbi wa mikutano katika makaazi ya wazee Sebleni inaendelea.

## D. UTEKELEZAJI WA MIRADI INAYOSIMAMIWA NA WIZARA

17. **Mheshimiwa Spika,** Wizara inatekeleza Miradi miwili ambao ni Mradi wa Hifadhi ya Wazee ambao ulipangwa kufanyia matengenezo majengo ya Wazee ya Sebleni Unguja na Limbani Pemba; na Mradi wa Maliza Vitendo vya Ukatili na Udhalilishaji wa Wanawake na Wasichana unaotekelezwa kwa mashirikiano na UNWOMEN.

18. **Mheshimiwa Spika,** Wizara tayari ishafunga mkataba na Mkandarasi aliyeshinda zabuni ya kufanya matengenezo ya majengo mawili machakavu na Ukumbi katika Makaazi ya Wazee Sebleni kwa kuanzia kulingana na bajeti iliyotengwa katika mwaka wa fedha 2023/2024. Mradi huu utaendelea katika mwaka wa fedha 2024/2025 kwa kuyahusisha majengo ya Wazee Limbani likiwemo suala la kujenga uzio wa eneo hilo.

19. **Mheshimiwa Spika,** Mradi wa Maliza Vitendo vya Ukatili na Udhalilishaji wa Wanawake na Wasichana ulianzishwa mwaka 2002 na niendelevu kwa kuzingatia Mipango ya Maendeleo ya Umoja wa Mataifa unatarajiwa kukamilika mwaka 2028. Mradi unalengo la kupinga Vitendo vya Udhalilishaji na unatekelezwa katika Wilaya zote za Zanzibar.

20. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka huu kupitia Mradi huo, Wizara imeandaa Mpango kazi wa Kitaifa wa Kupambana na Vitendo vya Ukatili na Udhalilishaji wa Wanawake na Watoto (2024 -2029) ambapo Mpango kazihuo kwa sasa uko katika hatua za kukamilishwa. Aidha, mradi umewawezesha watendaji wa Wizara kushiriki katika mikutano ya kimataifa ya Hali na Hadhi ya Wanawake duniani (CSW 68) na kufanya maadhimisho ya kimataifa ya Siku 16 za Kupinga Udhalilishaji na Siku ya Wanawake Duniani. Vile vile, Wizara imeanza hatua za kuandaa Sera ya Maendeleo ya Jamii na kufanya mapitio ya Sera ya Jinsia ya mwaka 2016.

## E. UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA PROGRAMU ZA FUNGU LA WIZARA

21. **Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo sasa naomba uniruhusu kutoa taarifa ya utekelezaji wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa mwaka wa fedha 2023/2024 kwa kuzingatia malengo yaliyowekwa kupitia programu mbali mbali.

22. **Mheshimiwa Spika,** shughuli zilizopangwa kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2023/2024 zilizingatia Sera, Sheria, Mikakati ya Kitaifa na Kimataifa, Ahadi za Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Maelekezo ya Serikali pamoja na Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi - CCM (2020-2025). Katika kipindi cha utekelezaji, Wizara ilijiwekea malengo katika maeneo yafuatayo: -

i. Kuanza utekelezaji wa shughuli zilizoainisha kwenye Mpango wa Ahadi za Kizazi Chenye Usawa;
ii. Kuongeza nguvu katika usimamizi wa miradi ya maendeleo;
iii. Kuimarisha nguvu kazi, kusimamia utendaji pamoja na kuandaa mazingira mazuri ya kazi;
iv. Kuimarisha mapambano dhidi ya vitendo vya ukatili na udhalilishaji kwa wanawake na watoto; na
v. Kuimarisha hifadhi ya jamii kwa wazee na watu wanaoishi katika mazingira magumu zaidi.

23. **Mheshimiwa Spika,** naomba sasa nielezee kwa kina utekelezaji wa programu kama ifuatavyo: -

**Programu ya Hifadhi ya Jamii**

24. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii ina jukumu la kuratibu na kusimamia upatikanaji wa haki kwa makundi

yenye mazingira magumu kwa kuimarisha mifumo ya hifadhi ya jamii na huduma kwa wazee, watoto na watu wanaoishi katika mazingira magumu zaidi ili kupunguza kiwango cha umasikini nchini. Shughuli za hifadhi ya jamii zinatekelezwa kwa kuzingatia mikakati ya Kitaifa na Kimataifa, Sheria ya Mtoto Nambari 6 ya mwaka 2011, Sheria ya Wazee Nambari 2 ya mwaka 2020 na Sera ya Hifadhi ya Jamii ya mwaka 2014.

25. **Mheshimiwa Spika,** programu hii ilipanga kutekeleza shughuli zifuatazo: -

i. Kutoa huduma za hifadhi na ustawi wa jamii kwa watu wenye mazingira magumu zaidi.
ii. Kuratibu uendeshaji wa Mpango wa Pensheni Jamii; na
iii. Kufanya matengenezo katika Makaazi ya wazee Limbani na Sebleni.

26. **Mheshimiwa Spika,** Programu imeendelea kutoa huduma za hifadhi ya jamii kwa kuendelea kuwatunza wazee katika makaazi ya Sebleni, Welezo na Limbani. Hadi kufikia Machi 2024, jumla ya Wazee 68 waliopo katika makaazi ya wazee Welezo 38 (wanawake 13 na wanaume 25), Sebleni 21 (wanawake 13 na wanaume wanane) na Limbani wazee tisa (wanawake watatu na wanaume sita), wanaendelea kupatiwa huduma za kiustawi ikiwemo chakula, mavazi, malazi, matibabu na fedha za kujikimu. **Kiambatanisho nambari 2 kinatoa ufafanuzi.**

27. **Mheshimiwa Spika,** Wizara kwa kushirikiana na wadau mbali mbali imeadhimisha Siku ya Wazee Duniani ambayo hufanyika ifikapo tarehe 1 Oktoba ya kila mwaka. Maadhimisho hayo yalifanyika katika Ukumbi wa Dkt. Ali Mohammed Shein, Tunguu. Mgeni Rasmi alikuwa Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Hussein Ali Mwinyi ambapo aliwakilishwa na Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Mheshimiwa Othman Masoud Othman. Kauli mbiu ya mwaka 2023 ilikuwa ni "Uthabiti wa Wazee kwenye Dunia yenye Mabadiliko".

28. **Mheshimiwa Spika,** uratibu wa mpango wa Pencheni Jamii kwa wazee waliofikia umri wa miaka 70 na kuendelea umefanyika kwa usajili wa wazee 30,317 (Unguja 17,914 na Pemba 12,403). Aidha, jumla ya wazee wapya 3,144 wamesajiliwa na 1,429 wamefariki na kuondolewa katika mpango huu. **Kiambatanisho nambari 3 kinatoa ufafanuzi.**

29. **Mheshimiwa Spika,** katika kuendelea kuimarisha utoaji wa huduma za kiustawi, Wizara imetengeneza vitambulisho vya wazee 11,814 kwa Unguja na Pemba (Unguja 7,901 na Pemba 3,913) kati ya vitambulisho 25,000 vilivyopangwa kuchapishwa. Vitambulisho hivi vinalenga kurahisisha upatikanaji wa huduma za kijamii ikiwemo huduma za usafiri, matibabu na msaada kwa wadau wanaoguswa na huduma za kiustawi. Aidha, vitambulisho vilivyobaki vitaendelea

kuchapishwa baada ya Wizara kuhakiki vyema walengwa waliokuwepo kwenye Mpango wa Pencheni Jamii.

30. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ilipokea jumla ya malalamiko 691 (Unguja 313 na Pemba 378) yanayohusu ukiukwaji wa haki za watoto na mivutano ya malezi, ili kuhakikisha kuwa haki za watoto zinapatikana kwa mujibu wa sheria na taratibu zilizopo. Malalamiko hayo yanahusisha matunzo ya watoto na mvutano wa malezi ambao huathiri zaidi watoto. **Kiambatanisho nambari 4 kinatoa ufafanuzi.**

31. **Mheshimiwa Spika,** huduma za nyumba salama kwa wahanga wa vitendo vya udhalilishaji na ukatili wa kijinsia zimeendelea kutolewa. Hadi kufikia Machi 2024, jumla ya wahanga 66, wakiwemo watoto 60 na watu wazima 6 (wanawake 50 na wanaume 16) walipokelewa kwa ajili ya hifadhi ya muda kutokana na matukio mbali mbali ya udhalilishaji yaliyowakuta. **Kiambatanisho nambari 5 kinatoa ufafanuzi**.

32. **Mheshimiwa Spika,** Kituo cha marekebisho ya tabia kwa watoto wanaokinzana na sheria kilipokea watoto 19 (wanawake 3 na wanaume 16). Mbali ya kupatiwa huduma ya kurekebisha tabia, watoto hao pia hupatiwa taaluma za stadi za maisha, ushauri nasaha na ufundi stadi. Aidha, ziara za kuwatembelea watoto waliohitimu mafunzo zilifanyika kwa lengo la kuona maendeleo yao.

Vile vile, Wizara inafanya tathmini ya kijamii kwa watoto watoto wanaokinzana na sheria na wale wanaofanyiwa matukio ya ukatili na udhalilishaji, ikiwa ni utekelezaji wa Sheria ya Mtoto. Jumla ya kesi 365 (Jinai 119 na Madai 246) zilifunguliwa Mahakamani ambapo kesi zilizotolewa hukumu ni 46. **Kiambatanisho nambari 6 kinatoa ufafanuzi.**

33. **Mheshimiwa Spika,** Wizara inaendelea kukisimamia kituo cha kulelea watoto Mazizini chenye jumla ya watoto 31 (wanawake 10 na wanaume 21). Aidha, Wizara imefuatilia vituo vya kulelea watoto 12 (Unguja 11 na Pemba 1) kwa lengo la kufuatilia huduma zinazotolewa katika vituo hivyo pamoja na kutoa ushauri na maelekezo kwa wasimamizi wa malezi ya watoto. **Kiambatanisho nambari 7 kinatoa ufafanuzi**.

34. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imefuatilia uendeshaji wa vituo 50 (Unguja 40 na Pemba 10) vya Malezi ya kutwa kwa watoto (Day Care Centres). Hatua hiyo ni kwa mujibu wa sheria na taratibu za Serikali. Aidha, taratibu za kuhamasisha uanzishwaji wa vituo zinaendelea ambapo mikutano ya wadau wa vituo vya makuzi na malezi ya awali ya mtoto (ECD) ilifanyika Unguja na Pemba. **Kiambatanisho nambari 8 kinatoa ufafanuzi**.

35. **Mheshimiwa Spika,** katika kusimamia mpango wa malezi ya nosh, jumla ya watoto 26 (wanawake 16 na wanaume 10) wameanza kupatiwa huduma ya malezi na

watoto wawili wameunganishwa na familia zao. Aidha, jumla ya walezi wa malezi 204 wamesajiliwa katika Mkoa wa Mjini Magharibi (74), Mkoa wa Kaskazini Unguja (42), Mkoa wa Kusini Pemba (38) na Mkoa wa Kaskazini Pemba (50).

36. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kutoa huduma za Ustawi wa Jamii kwa familia 204 (131 Unguja na 73 Pemba). Wizara pia imeendelea kutoa msaada wa akinamama 31 (Unguja 23 na Pemba 8) waliojifungua watoto pacha zaidi ya wawili. Vile vile, walengwa 48 (wanaume 24 na wanawake 24) wanaoishi katika kijiji cha Makundeni walipatiwa posho la shilingi 30,000 kwa kila kaya kwa mwezi. Misaada hii ni kwa ajili ya kuwawezesha kujikimu kimaisha.

37. **Mheshimiwa Spika,** Wizara inaendelea kutoa huduma za mazishi ambapo jumla ya maiti 11 (mwanamke mmoja na wanaume kumi) ambazo hazina ndugu zimezikwa na Serikali. Baadhi ya maiti hizo ni wazee waliokuwa wakiishi kwenye makaazi ya wazee Sebleni, Welezo na Limbani.

## Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara

38. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii ina jumla ya programu ndogo tatu ambazo ni Utawala na Uendeshaji, Uratibu wa Mipango, Sera na Utafiti; na Utawala na Uendeshaji Ofisi Kuu Pemba. Utekelezaji kupitia Programu ndogo hizo ni kama ifuatavyo: -

**Programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji**

**39. Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji ilipanga shughuli zifuatazo: -

i. Kuendelea kuwajengea uwezo watumishi wa Wizara;
ii. Kununua nyenzo pamoja na vifaa vya Wizara;
iii. Kuendelea kufanya mapitio na kurekebisha sheria, miongozo na kanuni za Wizara;
iv. Kuendelea kuweka mazingira mazuri kwa watumishi pamoja na kuwapatia maslahi yao; na
v. Ushiriki wa Wizara katika shughuli za Kikanda na Kimataifa.

**40. Mheshimiwa Spika,** Wizara katika kuwajengea uwezo watumishi wake inaendelea kuwapatia mafunzo ya muda mrefu watumishi 22 (wanawake 12 na wanaume kumi) katika vyuo mbali mbali ndani na nje ya nchi. Aidha, watumishi 17 (wanaume kumi na wanawake saba) walihudhuria mafunzo ya muda mfupi. Vile vile, Wizara ilitoa taaluma kwa watunza ghala wa makaazi ya wazee Welezo, Sebleni na kituo cha watoto Mazizini pamoja na kukagua kituo cha kurekebisha tabia za watoto wanaokinzana na sheria kilichopo Rahaleo. Katika kipindi hiki pia, Wizara ilipokea wanafunzi 60 kutoka vyuo mbali mbali vya elimu ya juu na kupatiwa mafunzo kwa vitendo. **Kiambatanisho nambari 9a na b vinatoa ufafanuzi.**

41. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ilipokea watumishi wapya tisa kutoka Taasisi tofauti za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na kupelekea kuwa na jumla ya watumishi 303 (Unguja 260; wanaume 88 na wanawake 172 na Pemba 43; wanaume 19 na wanawake 24). **Kiambatanisho nambari 10** kinatoa ufafanuzi. Pia, Wizara iliwapatia likizo na stahiki zao watumishi 80 na watumishi wanane wamefanyiwa marekebisho ya mishahara yao. Aidha, watumishi wanane (Unguja 5 na Pemba 3) wamestaafu kazi kwa mujibu wa Sheria na Kanuni za Utumishi wa Umma.

42. **Mheshimiwa Spika,** shughuli za kawaida za ukaguzi wa ndani zimefanyika kwa nia ya kuimarisha udhibiti wa rasilimali za Serikali. Vile vile, uhakiki wa familia 237 (Unguja 119 na Pemba 118) zinazoishi katika mazingira magumu zaidi na zinazopata posho la Serikali umefanyika. Aidha, matengenezo ya kawaida ya gari na vyombo vyote vya moto yamefanyika pamoja na kukata bima kwa ajili ya gari tisa, vespa nne, bajaji mbili na honda tisa.

43. **Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha uwajibikaji na utendaji wa Wizara unaimarika jumla ya vikao 15 vilifanyika; Kamati ya Uongozi vitatu, Kamati Tendaji tisa, vikao viwili vya Kamati ya Ukaguzi na kikao kimoja cha wafanyakazi. Aidha, vikao vitano vya Bodi ya Zabuni vilifanyika kwa ajili ya kupitia zabuni mbali mbali zilizowasilishwa kulingana na taratibu.

44. **Mheshimiwa Spika,** hati tatu za Mashirikiano (MOU) zimetayarishwa na kutiwa saini. Hati hizo ni pamoja na ya ujenzi wa jengo la makaazi ya wazee la Welezo, Hati ya Mashirikiano kati ya Wizara na Shirika la Qatar Charity kwa ajili ya kusaidia hali za Ustawi wa watu mbali mbali ikiwemo watoto yatima; na mkataba wa kodi ya Jengo la Ofisi. Aidha, Wizara imetoa habari zinazohusu matukio mbalimbali ambapo habari 134 zilitolewa kwenye mitandao ya kijamii na magazeti mbali mbali yakiwemo Gurdian na Zanzibar Leo.

45. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imeshiriki mikutano ya kitaifa, kikanda na kimataifa yenye mnasaba na maendeleo ya jamii kupitia Jukwaa la Kizazi Chenye Usawa (GEF), Mkutano wa Jumuiya ya Madola unaohusiana na kulinda Ustawi wa Wanawake na Watoto uliofanyika Nchini Uingereza na Maadhimisho ya Siku ya Mapambano dhidi ya Rushwa Barani Afrika yaliyofanyika Arusha.

### Programu ndogo ya Uratibu Mipango, Sera na Utafiti

46. **Mheshimiwa Spika** Programu hii inashughulikia kuratibu uandaaji, utekelezaji na usimamizi wa Sera, Miongozo, Mipango ya sekta pamoja na kufanya mapitio ya sheria, kanuni na sera zinazohitaji kufanyiwa marekebisho. Shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni hizi zifuatazo: -

i. Kufanya mapitio ya Sera, Kanuni na Muongozo;
ii. Kuratibu uandaaji wa mipango, ripoti za utekelezaji, tafiti na uchambuzi wa kisekta na utekelezaji wa shughuli za miradi ya maendeleo; na
iii. Kukusanya na kuchakata takwimu za sekta, matukio ya udhalilishaji na ustawi wa jamii pamoja na kuziwasilisha kwa wadau.

47. **Mheshimiwa Spika,** kupitia mashirikiano na Kijiji cha SOS, Rasimu ya Sera ya Mtoto imeandaliwa na kujadiliwa katika vikao vya wadau. Rasimu ya Sera hiyo kwa sasa tayari imeshawasilishwa kwenye Kamati ya Uongozi ya Wizara na inakamilishwa ili iwasilishwe kwa hatua zaidi. Aidha, mapitio ya Sheria ya Mtoto Nam. 6 ya mwaka 2011 yapo katika hatua ya kukamilishwa ili nayo iwasilishwe Serikalini.

48. **Mheshimiwa Spika,** mikutano miwili ya uanzishaji wa majukwaa ya uwezeshaji wanawake kiuchumi iliyofanyika kwa Makatibu Tawala wa Wilaya 11 Unguja na Pemba. Lengo la mikutano hiyo ni kutoa taarifa juu ya Mpango wa Serikali wa kuanzisha majukwaa ya kuwawezesha wanawake kiuchumi na kuwakabidhi jukumu la kuhamasisha wanawake kujiunga katika vikundi ambavyo ndio msingi wa majukwaa hayo. Aidha, Makatibu Tawala hao walihamasishwa kukusanya takwimu sahihi za vikundi vya wajasiriamali wanawake vilivyomo katika Wilaya husika.

49. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ilishiriki katika vikao vya awali vya utayarishaji wa Mpango Kazi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki katika masuala ya Wanawake, Amani na Usalama kilichofanyika Entebbe, Uganda na maandalizi ya kongamano la Kitaifa na Kimataifa la Wafanyabiashara wanawake kwenye Eneo Huru la Biashara Barani Afrika (AfCFTA) lililofanyika Dar es Salaam. Aidha, maafisa mipango walishiriki kikao cha wadau wa maendeleo wanaohusiana na utekelezaji wa masuala ya Jinsia pamoja na Mkutano wa Bajeti Jumuishi zinazozingatia Usawa wa Kijinsia (Gender Responsive Budget) vilivyofanyika Zanzibar.

50. **Mheshimiwa Spika,** Mradi wa Kukuza Usawa wa kijinsia Tanzania (PAMOJA), ambao utatekelezwa kwa muda wa miaka mitano (2024 – 2028) umetayarishwa. Mradi huo unategemewa kuanza mwaka wa fedha 2024/2025 na watekelezaji ni Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kwa Tanzania Bara na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa Zanzibar. Aidha, Zanzibar imetengewa shilingi 33,800,000,000.00 kupitia mkopo wa Benki ya Dunia na ruzuku shillingi 1,300,000,000.00. Mradi huo unalenga katika maeneo makuu matatu; Kuwawezesha wanawake kiuchumi: Kupinga na kukabiliana na vitendo vya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia: na Ubunifu na ushirikishwaji. Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto inatekeleza mradi huu kwa kushirikiana na Wakala wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (ZEEA).

51. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imeshirikiana na Ofisi ya Rais Fedha na Mipango katika kuandaa Bajeti inayozingatia Usawa wa Kijinsia kwa Wizara sita kwa kuanzia. Wizara hizo ni Afya; Elimu na Mafunzo ya Amali; Uchumi wa Buluu na Uvuvi; Kilimo, Umwagiliaji, Mifugo na Mali asili na Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumuishi wa Umma na Utawala Bora. Ni malengo ya Serikali kuhakikisha kuwa Wizara zote zinatayarisha na kutekeleza mpango na bajeti inayozingatia jinsia kuanzia mwaka 2025/2026. Mafunzo ya Bajeti Jumuishi inayozingatia Usawa wa Kijinsia yametolewa kwa maafisa Mipango na Mtambuka wanaoshughulikia masuala ya Jinsia (wanawake kumi na wanaume saba) wa Wizara 10 za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar zilizobakia. **Kiambatanisho nambari 11 kinatoa ufafanuzi.**

**Programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji Ofisi Kuu Pemba**

52. **Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo hii inahusika na uratibu wa masuala yote yanaohusu majukumu ya Sekta ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa upande wa Pemba ambapo hadi kufikia Machi, 2024 shughuli zifuatazo zilitekelezwa: -

   i. Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa shughuli za Wizara;
   ii. Kuendelea kuwajengea uwezo watumishi wa Wizara, Pemba;

iii. Kuendelea kuratibu na kusimamia utekelezaji wa sera, sheria, miongozo na kanuni za Wizara; na
iv. Kuendelea kuweka mazingira mazuri kwa watumishi pamoja na kuwapatia maslahi yao.

53. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi Kuu Pemba iliratibu ziara za Viongozi wa Wizara kisiwani Pemba pamoja na kushiriki ziara na mikutano mbali mbali ya Viongozi Wakuu wa Kitaifa wa Serikali. Aidha, ofisi ilifanya ziara za ufuatiliaji katika vikundi vya wajasiriamali wanawake, vituo vya kulelea watoto na Makaazi ya Wazee. Ziara hizo ziliratibiwa kwa lengo la kubaini mafanikio na changamoto zilizopo katika maeneo hayo. Kupitia ziara na mikutano hiyo miongozo, maelekezo na ushauri uliotolewa na kupokelewa. Vile vile, Ofisi Kuu Pemba imeimarisha upatikanaji wa huduma na vitendea kazi na kuweka mazingira bora ya ofisi.

## Programu ya Maendeleo ya Jamii na Jinsia

54. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii inahusika na jukumu la kuratibu na kusimamia utekelezaji wa haki za Wanawake, Wanaume na Watoto ikiwa ni pamoja na kusimamia utekelezaji wa Sera na Sheria zinazohusu Maendeleo ya Jamii kwa kuzingatia Mipango ya Kitaifa, Mikataba ya Kikanda na Kimataifa. Shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni kama zifuatazo: -
i. Kusimamia na kuendeleza juhudi za kukuza usawa wa kijinsia na uwezeshaji wa wanawake;

ii. Kuendeleza mapambano dhidi ya vitendo vya ukatili na udhalilishaji kwa wanawake na watoto;
iii. Kujenga uwezo na ushiriki wa watoto katika mabaraza ya watoto; na
iv. Kusimamia shughuli za maendeleo ya jamii.

55. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imo katika hatua za kutayarisha Mpango Kazi mpya wa Kitaifa wa Kupambana na Vitendo vya Ukatili na Udhalilishaji wa Wanawake na Watoto (NPA VAWC 2023 -2028). Hatua iliyofikiwa ni kuandaliwa kwa rasimu ya mwanzo ya mpango huo kwa kushirikiana vikao na wadau mbalimbali. Makundi yaliyohusika katika kutoa maoni ni pamoja na wanawake, watoto, wizara mbali mbali, asasi za kiraia pamoja na Makatibu na Naibu Makatibu Wakuu.

56. **Mheshimiwa Spika,** Utafiti wa ustawi na Afya ya Vijana na Watoto Tanzania unafanyika ukiwa katika hatua ya ukusanyaji wa taarifa katika kaya kwenye Mikoa yote ya Tanzania Bara na Zanzibar. Kazi hii inafanyika kwa mashirikiano na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum ya Tanzania Bara, Ofisi za Takwimu (OCGS & NBS), Tanzania Health Promotion Support (THPS) na UNICEF. Lengo la utafiti huo ni kuangalia na kutathmini afya, ustawi wa jamii na uzoefu wa Maisha kwa vijana wa Tanzania. Utafiti huu unawahusisha wakuu wa kaya na vijana wa miaka 13 – 24 wa kike na wa kiume. Ni imani ya

Wizara kuwa utafiti huu utakapomaliza matokeo yake yatasaidia Serikali katika kuboresha sera, kupanga mipango, programu na huduma zinazohusu maendeleo ya vijana nchini.

57. **Mheshimiwa Spika,** Wizara kwa kushirikiana na wadau wanaoshughulikia masuala ya Haki za Wanawake iliandaa ripoti ya Hali na Hadhi ya Wanawake (CSW68), iliyowasilishwa Makao Makuu ya Umoja wa Mataifa Marekani mwezi Machi 2024. Ripoti hiyo Ujumbe wa mkutano huo wa 68 ulikuwa "Kupunguza Umaskini na kuwezesha Wanawake kiuchumi kwa kuzingatia usawa wa kijinsia kwa taasisi zote".

58. **Mheshimiwa Spika,** mkutano mkuu wa mwaka 2023 wa Bodi ya Ushauri ya Watoto Zanzibar (NCAB) umefanyika kwa ushirikiana na Shirika la Mtandao wa Haki za Watoto Zanzibar (Zanzibar Child Rights Forum) na Save the Children. Pamoja na mambo mengine mkutano ulitathmini utekelezaji wa shughuli za bodi na kupitia mpango kazi wa mwaka 2024. Vile vile, Muongozo wa uanzishaji na uendeshaji wa Mabaraza na Klabu za Watoto umeandaliwa ili kuimarisha utekelezaji wa majukumu ya mabaraza. Jumla ya washiriki 66 (wanawake 43 na wanaume 23) wameshiriki vikao hivyo Unguja na Pemba.

59. **Mheshimiwa Spika,** Muongozo wa Majukwaa ya Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi umetayarishwa kwa

lengo la kutoa fursa ya kuwainua Wanawake kiuchumi, biashara, upatikanaji wa mitaji, matumizi ya teknlojia na uzalishaji wa ajira. Aidha, Majukwaa yanadhamira ya kuwakutanisha wanwake ili waweze kuiba fursa za kiuchumi, kuzitumia pamoja kujadili na kutatua changamoto mbali mbali wanaozokutana nazo.

60. **Mheshimiwa Spika,** mikutano ya uhamasishaji wa vikundi vya wanawake imefanyika katika wilaya zote za Unguja na Pemba. Katika mikutano hiyo wanawake walibainishwa kwamba ngazi ya msingi ya majukwaa ni vikundi vilivyoanzishwa katika ngazi za jamii (Shehia) na kwamba kutakuwa na Majukwaa ngazi ya Wilaya, Mikoa na Taifa. Jumla ya vikundi 1,136 vilishiriki katika mikutano hiyo (Unguja vikundi 455 na Pemba vikundi 681). Aidha, jumla ya wanawake walioshiriki ni 34,080 (Unguja 13,650 na Pemba 20,430). **Kiambatanisho nambari 12 kinatoa ufafanuz**i.

61. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imewaunganisha wanawake wajasiriamali 50 katika mafunzo ya wiki moja ya utengezaji wa batiki kwa vikundi vya wanawake wajasirimali ili kujiajiri wenyewe na kujikwamua na umasikini. Aidha, Wizara imevipatia fursa vikundi 14 vya wanawake wajasiriamali kushiriki katika maonesho ya Siku ya Chakula Duniani yaliyofanyika Chamanangwe Pemba. Vikundi vilivyoshiriki vilitoka katika Wilaya za Chake Chake, Mkoani, Wete na Micheweni. Lengo la ushiriki huo ni kupata kujitangaza na kutafuta fursa za kibiashara.

62. **Mheshimiwa Spika,** jumla ya malalamiko 16 yaliyowasilishwa na wanawake yamepokelewa ambapo kati ya hayo malalamiko manane yanahusiana na kupigwa na manane yanahusiana na madai ya makaazi. Kati ya malalamiko hayo tisa yamepatiwa ufumbuzi, malalamiko matano yalipatiwa rufaa kwenda mahakamani na mawili yanaendelea kutafutiwa ufumbuzi. **Kiambatanisho nambari 13 kinatoa ufafanuzi.**

63. **Mheshimiwa Spika,** jumla ya simu za malalamiko 877 ya Ukiukwaji wa Haki za Watoto zimepokelewa kupitia huduma ya simu kwa Mtoto Zanzibar (C-SEMA) ambapo Simu 25 zilihusisha taarifa za udhalilishaji wa kingono (ubakaji), udhalilishaji wa kimwili, madai ya matunzo ya Watoto, kupata taarifa kuhusu Huduma ya Simu kwa Mtoto na haki ya Mtoto.

64. **Mheshimiwa Spika,** jukwaa lamashauriano linalohusisha Taasisi za Serikali na Asasi za Kiraia zikiwemo Mahakama, Jeshi la Polisi, Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka, Vituo vya Mkono kwa Mkono, ZAFELA, ANGOZA na wadau wa maendeleo limeanzishwa. Lengo kuu ni kuwezesha kutatua changamoto za vitendo vya ukatili wa kijinsia. Miongoni mwa maazimio ya Jukwaa hilo ni pamoja na kuweka mkakati wa kuendelea kuimarisha utendaji na utoaji wa huduma kwa walengwa ili haki iweze kufikiwa.

65. **Mheshimiwa Spika,** hatua za kuelimisha na kuhamasisha jamii juu ya mapambano dhidi ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia zimechukuliwa kwa kushirikiana na Viongozi wa Dini, Waratibu wa Wanawake na Watoto wa Shehia na Wasaidizi wa Sheria. Jumla ya Shehia 61 (Unguja 46 na Pemba 15), skuli 45 (Unguja 15 na Pemba 30) na madrasa 24 (Unguja 16 na Pemba 8) zimpatiwa elimu hiyo. Aidha, tathmini na ufuatiliaji kwa Timu za Wilaya za Viongozi wa Dini imefanyika ambapo washiriki 88 (Unguja 55 na Pemba 33) walihudhuria. Viongozi hao wa Dini waliwasilisha taarifa zao za utekelezaji na mipango kazi yao.

66. **Mheshimiwa Spika,** Wizara kwa kushirikiana na taasisi ya ZAYADESA imewaunganisha Baba Bora watano kwa ajili ya mafunzo. Kati ya Baba Bora hao watatu ni kutoka Wilaya ya Kati na wawili ni kutoka Wilaya ya Magharibi "A". Vile vile, familia 27 zimepatiwa ushauri nasihi kwa ajili ya kukabiliana na matukio mbali mbali ya udhalilishaji. Aidha, mikutano ya kutoa elimu kupitia Timu ya Wanaume wa Mabadiliko (Male Champions) katika Wilaya za Chake chake, Wete na Mkoani. Jumla ya washiriki wanaume 120 walishiriki katika Mikutano hiyo yenye lengo la kutoa elimu, kubadili mitazamo na kubadilishana mawazo na makundi rika ya vijana na wazee wa kiume katika kuwashajihisha kushiriki kikamilifu katika kupinga vitendo vya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia.

67. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imefanya vikao na Waratibu wa Wanawake na Watoto wa Shehia katika Wilaya zote za Unguja na Pemba. Lengo la vikao hivyo ni kuwasilisha ripoti za utekelezaji, kubadilishana uzoefu pamoja na kuimarisha utendaji katika utoaji wa huduma kwa wanawake na watoto katika Shehia zao. Aidha, vikao na waratibu na Masheha wa Wilaya ya Kati na Kaskazini A na B vimefanyika vyenye lengo la kuwaunganisha Masheha na Waratibu wa Shehia zao ili kusimamia shughuli za kimaendeleo.

68. **Mheshimiwa Spika,** kupitia vyombo vya habari elimu ya kujikinga na vitendo vya ukatili na udhalilishaji imetolewa kwa kuandaa na kurusha vipindi vya Redio na Televisheni pamoja na makala. Jumla ya vipindi 28 vya Redio, 22 Televisheni na Makala 10 vilitayarishwa na kurushwa hewani. **Kiambatanisho nambari 14 kinatoa ufafanuzi.**

69. **Mheshimiwa Spika,** Wizara kwa kushirikiana na Shirika la UNESCO imefanya warsha ya mapitio ya Muongozo wa Malezi na Mawasiliano kati ya Wazazi/Walezi na Watoto kwa wadau, wakiwemo WEMA, Tume ya UKIMWI, BAKIZA, Chuo kikuu cha SUMAIT, ZAPHA+ n.k. Lengo la warsha hiyo ni kuimarisha muongozo huo kwa kuweka mawazo chanya yanayokidhi mahitaji ya sasa. Aidha, Muongozo huo tayari umesharidhiwa na upo tayari kwa ajili ya matumizi.

70. **Mheshimiwa Spika,** Wizara kwa kushirikiana na Asma Mwinyi Foundation imegawa taula za kike kwa wanafunzi 4,200 (Unguja 2,180 na Pemba 2,020) ili kuwawezesha kushiriki katika shughuli za masomo yao kwa ufanisi na kuwapunguzia makali ya maisha. Taasisi hiyo pia imetoa msaada wa vyakula na vifaa kwa Skuli ya Hasnuu Makame baada ya kupata janga la kuunguliwa na moto.

71. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imefanya maadhimisho ya siku 16 za harakati za kupinga vitendo vya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia, Siku ya Mtoto wa Kike na Siku ya Wanawake Duniani. Maadhimisho hayo yalijumuisha mikutano, warsha na makongamano. Lengo kuu la maadhimisho hayo ni kuongeza uelewa wa jamii na uchukuaji wa hatua ikiwa ni utekelezaji wa mikataba ya Kimataifa ambayo Tanzania imeridhia. Aidha, Wizara imetoa zawadi kwa wanawake 200 (Unguja 120 na Pemba 80) waliojifungua siku ya wanawake duniani katika Hospitali za Kivunge, Makunduchi na Mwembeladu kwa Unguja na Vitongoji, Micheweni na Kinyasini Pemba ili kuwasaidia wanapofika nyumbani.

## F. MWELEKEO WA BAJETI YA WIZARA KWA MWAKA 2024/2025

### a. Malengo ya Wizara kwa mwaka 2024/2025

72. **Mheshimiwa Spika,** mwelekeo wa utekelezaji wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa mwaka wa fedha 2024/2025 umezingatia maelekezo yaliyotolewa na Serikali ya Awamu ya Nane katika kuimarisha utoaji wa huduma. Wizara itahakikisha kwamba huduma zinaendelea kuimarishwa pamoja na kutia nguvu zaidi kupambana na vitendo vya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia na kustawisha jamii. Kwa muktadha huo, vipaumbele vya Wizara vinagusa maeneo yafuatayo: -

i. Kuimarisha usimamizi wa shughuli za Wizara ikiwemo kutayarisha na kufanyia mapitio zana za kufanyia kazi za masuala ya maendeleo ya jamii, jinsia, wazee na watoto;
ii. Kuimarisha nguvu kazi na mazingira mazuri ya kazi ikiwemo upatikanaji wa vitendea kazi, matengenezo ya majengo na kuimarisha kumbukumbu muhimu za kiutumishi;
iii. Kuratibu utekelezaji wa sera, tafiti, miongozo, sheria, na kanuni;
iv. Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Ahadi za Nchi za Kizazi Chenye Usawa na uwezeshaji wanawake kiuchumi; na

v. Kuimarisha Hifadhi ya Jamii, Wazee, Watoto na Familia zinazoishi katika mazingira magumu zaidi pamoja na kuratibu na kusimamia huduma za Pencheni Jamii.

**b. Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa mwaka 2024/2025**

**73. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2024/2025 Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto imekadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 12,000,000.00 kuchangia mfuko Mkuu wa Serikali.

**c. Mwelekeo wa Matumizi kwa Programu**

**74. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2024/2025 Wizara imekadiriwa kutumia jumla ya shilingi 23,315,462,000.00. Kati ya fedha hizo shilingi 9,959,836,000.00 ni za Matumizi ya Kawaida zinazohusisha shilingi 3,888,989,999.00 za Mishahara na shilingi 6,073,837,000.00 za Matumizi Mengineyo. Kati ya Fedha za Matumzi Mengineyo, shilingi 4,384,201,000.00 ni kutoka SMZ, shilingi 1,189,636,000.00 zinatoka kwa Mshirika wa Maendeleo UNICEF na 500,000,000.00 kwa ajili ya uratibu wa Usawa wa kijinsia. Aidha, fedha za Miradi ya Maendeleo ni shilingi 13,355,626,000.00 zinazojumuisha fedha kutoka Serikalini 4,500,000,000.00, Ruzuku za Washirika wa Maendeleo (UNWOMEN) shilingi

536,000,000.00, UNFPA 208,000,000.00 na shilingi 8,111,626,000.00 ni Mkopo kutoka Benki ya Dunia. **Angalia kiambatanisho Nambari 15 kwa ufafanuzi zaidi.**

**Programu ya Hifadhi ya Jamii (PH0401)**

**75. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Wizara imepanga kutumia shilingi 5,798,835,000.00 sawa asilimia 25 ya bajeti ya Wizara. Kupitia Programu hii Wizara imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo: -

i. Kuendelea kuwahudumia Wazee wanaoishi katika nyumba za Wazee Unguja na Pemba; Kuwafuatilia na kuwafikia wazee wanaostahiki kuingia katika Mpango wa Pencheni Jamii na kuwapatia vitambulisho vitakavyowasaidia kupata huduma za jamii;
ii. Kuendelea kufanya matengenezo katika makaazi ya wazee Sebleni na Limbani, kujenga upya makaazi ya wazee ya Welezo na kununua samani kwa ajili ya makaazi hayo; na
iii. Kutoa huduma za hifadhi na ustawi wa jamii kwa watu wenye mazingira magumu zaidi.

**Programu ya Utawala na Uendeshaji (PH0402)**

**Programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji**

76. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Wizara imepanga kutumia shilingi 4,738,047,000.00 sawa asilimia 20 ya bajeti ya Wizara. Kupitia Programu hii shughuli zitakazotekelezwa ni pamoja na:

   i. Kuendelea kuwajengea uwezo watumishi wa Wizara na kuwapatia maslahi yao;
   ii. Kutekeleza shughuli za uendeshaji wa Ofisi ikiwa ni pamoja na kuipatia Wizara vitendea kazi; na
   iii. Kuendelea kuimarisha kumubukumbu na nyenzo nyingine za kiutumishi ili kuweka usimamizi imara wa rasilimali watu katika Wizara.

**Programu ndogo ya Uratibu wa Mipango, Sera na Utafiti**

77. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Wizara imepanga kutumia shilingi 8,992,763,000.00 sawa asilimia 39 ya bajeti ya wizara. Shughuli zitakazotekelezwa pamoja na:

   i. Kuratibu utayarishaji wa Mipango, Bajeti, na Ripoti za Wizara;
   ii. Kuandaa na kuchambua sera zinazosimamiwa na Wizara na Sera nyingine za Kisekta ili kuhakikisha dhana ya maendeleo ya jamii na mipango na bajeti

inayozingatia jinsia zinaendelea kukondoeshwa;

iii. Kuimarisha mfumo wa ufuatiliaji na tathmini kwa kuzingatia uratibu wa masuala yote yanayosimamiwa na Wizara ikiwemo uratibu wa bajeti inayozingatia Jinsia utaimarishwa sambamba na kufanya tafiti; na

iv. Kuratibu utekelezaji wa Miradi yote ya Wizara ukiwemo Mradi wa Kukuza Usawa wa Kijinsia (PAMOJA).

**Programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji Ofisi Kuu Pemba**

**78. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Wizara imepanga kutumia shilingi 1,402,704,000.00 sawa asilimia 6 ya bajeti ya Wizara. Kupitia programu hii, yafuatayo yamepangwa kutekelezwa: -

i. Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa shughuli za Wizara Pemba;

ii. Kuendelea kuratibu na kusimamia utekelezaji wa sera, sheria, miongozo na kanuni za Wizara; na

iii. Kuendelea kuwajengea uwezo watumishi kuweka mazingira mazuri pamoja na kuwapatia maslahi yao.

**Programu ya Maendeleo ya Jamii na Jinsia (PH0403)**

**79. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Wizara imepanga kutumia shilingi 2,392,112,000.00 sawa na asilimia 10 ya bajeti ya Wizara. Programu ya

Maendeleo ya Jamii na Jinsia imepanga kutekeleza yafuatayo: -

i. Kuratibu, kusimamia na kutekeleza mpango kazi mpya wa kupambana na vitendo vya ukatili na udhalilishaji wa wanawake na watoto (NPA-VAWC 2024-2029);
ii. Kuandaa Sera ya Maendeleo ya Jamii pamoja na miongozo ya utoaji wa huduma za maendeleo ya jamii na kukamilisha tathmini ya utekelezaji wa sera ya jinsia;
iii. Kuratibu na kuhamasisha utekelezaji wa Ahadi za Nchi juu ya Kizazi Chenye Usawa;
iv. Kuratibu, kuwawezesha na kuwaunganisha wanawake na fursa mbali mbali;
v. Kuratibu, kuwezesha na kuimarisha mabaraza ya watoto katika ngazi zote; na
vi. Kuhamasisha na kuimarisha malezi ya pamoja.

## G. SHUKURANI

80. **Mheshimiwa Spika,** mashirikiano mazuri na Taasisi za Serikali na zisizo za Serikali, mashirika ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa, Sekta binafsi na mtu mmoja mmoja ndio chachu ya mafanikio yaliyofikiwa na Wizara. Kwa niaba ya Serikali, Wizara inatambua na kuthamini michango yao wanayoitoa katika kufanikisha malengo ya Wizara na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa ujumla. Wizara hii inasimamia masuala

mtambuka kwa Wizara zote na ni dhahiri kuwa dhana nzima ya utoaji wa huduma na maendeleo ya jamii, kulinda ustawi wa jamii (wanawake, wanaume, wazee na watoto), pamoja na kupinga na kupambana na vitendo vyote vya ukatili na udhalilishaji dhidi ya wanawake na watoto vinahitaji nguvu za pamoja. Kwa niaba ya Wizara natoa shukurani za dhati kwa wote walioshirikiana nasi katika utekelezaji wa shughuli kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

81. **Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa shukurani za pekee kwa Chama cha Mapinduzi (CCM) na Jumuiya zake kwa kusimamia vyema utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020 – 2025. Aidha, ninazishukuru Wizara zote za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa mashirikiano yao waliyoipatia Wizara yangu katika mwaka wa fedha 2023/2024. Nap¬¬¬¬¬enda kuishukuru Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mashirikiano wanayotupatia pamoja na Ofisi ya Makamu wa Rais na Wizara mbali mbali za Serikali ya Muungano wa Tanzania. Aidha, naishukuru kwa dhati Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT) na Kamati ya Kitaifa ya Mapambano ya Vitendo vya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia ya UWT.

82. **Mheshimiwa Spika,** Wizara yangu inatoa shukurani kwa Washirika wa Maendeleo na Mashirika ya

Kimataifa kama ifuatavyo: - Ofisi za Ubalozi Mdogo wa China uliopo Zanzibar, Umoja wa Falme za Kiarabu - UAE, Umoja wa Ulaya - EU, Qatar Foundation, World Bank, UNICEF, UNFPA, UNWOMEN, UNESCO, WHO, HelpAge International, SOS, IOM, USAID, Save the Children na CDC. Ninazishukuru taasisi mbalimbali za SMZ na SMT zikiwemo Benki ya Watu wa Zanzibar - PBZ, NMB, CRDB, Benki ya AZANIA, ZURA, Mamlaka ya Mapato Tanzania - TRA, Mamlaka ya Mapato Zanzibar - ZRA, TIRA, Shirika la Bandari Zanzibar - ZPC, Afisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali, SUZA, ZU, Chuo cha Maendeleo ya Jamii Tengeru na Chuo Kikuu cha SUMAIT. Wizara yangu pia imeshirikiana na Taasisi za Sheria ikiwemo Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka, Mahakama, Jeshi la Polisi na ZAECA. Ninatambua pia mchango wa taasisi ya LSF, Action Aid, Pathfinder, THPS, Step Up Foundation, Nuru Foundation, Noah Foundation and Good People, Mabaraza ya Wazee, JUWAZA, JUYAWAZA, TAMWA, ZAFELA, C-Sema, ZASWA, CRF, ZAMWASO, ZASO, ZACA, ZAPHA+, BAKIZA, Park Hayatt Hotel, THESODE, Zanzibar Maisha Bora Foundation, Mwanamke Initiative Foundation, Daraja Foundation, Asma Mwinyi Foundation, Assalam Foundation, Sino Youth Africa, Community Forest Pemba, Zanzibar Vijana Vision Group na Mrajis wa NGO Zanzibar. Natumia fursa hii kuwashukuru wale wote ambayo sikuweza kuwataja katika taarifa hii na naomba watambue kuwa mchango wao tunauthamini

sana. Kuwashukuru Waandishi wa Habari, Vikosi vya Ulinzi na Usalama vya SMT na SMZ zikiwemo JKU, Uhamiaji (Zanzibar) na Wakuu wa Mikoa, Wilaya, Madiwani na Masheha wote.

83. **Mheshimiwa Spika,** natoa shukurani za dhati kwa Uongozi na Watumishi wote wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa mashirikiano wanayonipa. Ninamshukuru Naibu Waziri, Mheshimiwa Anna Athanas Paul. Hakika ananipa ushirikiano mkubwa katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara. Ninamshukuru Katibu Mkuu, Ndugu Abeida Rashid Abdallah na Naibu Katibu Mkuu Ndugu Khatib Mwadini Khatib, ambao kwa hakika wanafanya kazi kubwa ya kuiongoza Wizara yetu kiutendaji. Natambua mchango wa Afisa Mdhamini, Ndugu Hafidh Ali Mohamed Shoka na Wakurugenzi wote. Natoa shukurani za dhati Wakuu wa Divisheni, Wakuu wa Vitengo, Madereva pamoja na watumishi wote wa Wizara kwa ujumla. Mchango wao ni muhimu katika uhai na ustawi wa Wizara yetu. Nawashukuru Timu ya kusaidia Mapambano dhidi ya Ukatili na Udhalilishaji wakiwemo; Waratibu wa Wanawake na Watoto wa Shehia, Viongozi wa Dini, Masheha, Timu za Wanaharakati, Wasaidizi wa Sheria, Vituo vya Mkono kwa Mkono pamoja na Timu ya Wanaume wa Mabadiliko. Hakika wao ni kiunganishi muhimu baina ya Wizara na Wananchi katika maeneo mbalimbali.

**84.** **Mheshimiwa Spika,** naomba nimalizie kwa kuishukuru familia yangu kwa kunivumilia na kuniunga mkono katika kutekeleza majukumu yangu ya kila siku ya kiuongozi katika Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto. Mwenyezi Mungu awazidishie moyo wa ustahamilivu na kheri nyingi, Amin.

## H. HITIMISHO

**85.** **Mheshimiwa Spika,** naomba nimalizie kwa kufanya marejeo ya maeneo ambayo Wizara yangu inayasimamia. Maendeleo ya Jamii ni nguzo muhimu ya kuleta maendeleo katika nchi yetu. Ili kuitekeleza kivitendo dhana hii, Wizara yangu imo katika utaratibu wa kuanda Sera ya Maendeleo ya Jamii itakayokuwa dira ya kutuelekeza katika kuimarisha misingi ya kuwawezesha watu katika jamii kuwa ndio msingi na wanufaika wa maendeleo. Natoa shukurani za kipekee kwa Serikali yetu ya Awamu ya Nane chini ya Rais wetu mpendwa, Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi kulipa kipaumbele suala la Maendeleo ya Jamii kwa kuunda Wizara inayolisimamia. Katika kuwezesha dhamira ya maendeleo inafikiwa, Viongozi wetu wamekuja na ubunifu wa kumuweka mwanamke katika nafasi ya kipekee na kudhamiria kumuwezesha kupitia mpango wa Kizazi chenye Usawa (GEF). Mbali na kumuweka mwanamke katika nafasi ya kipekee, Wizara hii inasimamia haki mtambuka za mtoto ambaye ndiyo nguzo ya taifa letu. Malezi bora ya mtoto, lishe

bora, elimu bora na makuzi yenye stara kulingana na mila na silka za Kizanzibari ndiyo lengo letu. Jukumu hili linafanywa kupitia sekta mbali mbali na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto ndiyo yenye zana za msingi za kusimamia na kuhakikisha kuwa mtoto wa kizanzibari anaishi katika mazingira bora yatakayompelekea kuwa baba na mama bora wa baadaye.

86. **Mheshimiwa Spika,** sambamba na majukumu haya, Wizara hii inasimamia matunzo kwa wazee wetu ambao wameitumikia nchi hii kwa upendo mkubwa wakati wakiwa vijana katika nyanja mbali mbali. Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto inaendelea kuwatayarishia vitambulisho Wazee wetu ili waweze kupata huduma bora katika vyombo vya usafiri wa umma, huduma za afya na kwengineko. Masuala haya yanayosimamiwa na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, wazee na Watoto yanatuhusu sote hivyo ni wajibu wetu kuitikia wito wa kujenga kizazi chenye usawa kwa kuzingatia namna tunavyoweka mazingira wezeshi kwa wanawake na wanaume kujenga uchumi imara zaidi kwao binafsi, familia zao na hata taifa kwa ujumla. Tafiti zimebainisha kuwa nchi zinazozingatia usawa wa kijinsia zimeweza kuimarika kiuchumi kwa kasi kuliko nchi ambazo hazizingatii usawa huo.

**87.** **Mheshimiwa Spika,** naomba Wajumbe wa Baraza lako tukufu waichangie hotuba hii, watushauri ipasavyo na hatimaye waiidhinishie Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto matumizi ya **shilingi 23,315,462,000.00** ili kutekeleza kazi za kawaida na kazi za maendeleo kwa mwaka wa fedha 2024/2025, kwa mchanganuo uliotolewa. Aidha, Mheshimiwa Spika, naliomba Baraza lako tukufu liikubalie Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto ichangie kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali jumla ya **shilingi 12,000,000.00** zitakazokusanywa kupitia Idara ya Ustawi wa Jamii na Wazee.

| **Eneo la Matumizi/Chanzo** | **Kiasi** |
|---|---|
| Mishahara | **3,895,000,000** |
| Matumizi Mengineyo | **6,021,636,000** |
| Serikali | 4,384,201,000 |
| GEF | 500,000,000 |
| UNICEF | 1,189,636,000 |
| Kazi za maendeleo | **13,355,626,000** |
| Serikali | 4,500,000,000 |
| World Bank (PAMOJA Project) | 8,111,626,000 |
| UNFPA | 208,000,000 |
| UNWOMEN | 536,000,000 |
| **Jumla** | **23,315,462,000** |

**88. Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa hoja.

.............................

**RIZIKI PEMBE JUMA (MBM)**
**WAZIRI MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO**
**ZANZIBAR.**

**Kiambatanisho Nam. 1: Muhtasari wa Upatikanaji wa Fedha kwa Kipindi cha Julai, 2023 - Machi 2024**

| Idara/Programu | Fedha zilizopangwa | | | Fedha zilizopatikana | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Jumla | Mishahara | Matumizi Mengineyo | Jumla | % | Mishahara | % | Matumizi Mengineyo | % |
| Programu ya Hifadhi ya Jamii | 956,974,000 | - | 956,974,000 | 488,504,579 | 51 | - | - | 488,504,579 | 51 |
| Programu ya Utawala na Uendeshaji | 4,238,723,500 | 2,891,370,000 | 1,347,353,500 | 2,760,914,016 | 65 | 2,350,555,195 | 81 | 410,358,821 | 30 |
| | 381,515,000 | - | 381,515,000 | 69,264,500 | 18 | - | - | 69,264,500 | 18 |
| | 1,028,630,260 | 278,630,000 | 750,000,000 | 457,832,356 | 45 | 389,902,749 | 140 | 69,264,500 | 18 |
| Programu ya Maendeleo ya Jamii na Jinsia | 564,157,500 | - | 564,157,500 | 392,128013 | 70 | - | - | 392,128013 | 70 |
| Fedha za Maendeleo (SMZ) | 1,500,000,000 | - | - | - | - | - | - | - | - |
| Fedha za Maendeleo (UNWOMEN) | 636,321,000 | - | - | 279,018,672 | 44 | - | - | - | - |
| Fedha za Wahisani (UNFPA) | 300,990,000 | - | 300,990,000 | 256,358,404 | 85 | - | - | 256,358,404 | 85 |
| Fedha za Wahisani (UNICEF) | 280,000,000 | - | 280,000,000 | 58,726,700 | 21 | - | - | 58,726,700 | 21 |
| **JUMLA KUU** | **9,887,311,260** | **3,170,000,000** | **4,580,990,000** | **4,506,388,835** | **46** | **2,740,457,944** | **86** | **1,765,930,891** | **39** |

**Chanzo: WMJJWW, 2023/24**

**Kiambatanisho Nam. 2: Makaazi ya Wazee Unguja na Pemba**

| Kituo | Idadi ya Wazee | | Jumla |
|---|---|---|---|
| | KE | ME | |
| 1. Sebleni | 13 | 08 | 21 |
| 2. Welezo | 13 | 25 | 38 |
| 3. Limbani (Pemba) | 03 | 06 | 09 |
| **JUMLA** | **29** | **39** | **68** |

**Chanzo: WMJJWW, 2023/24**

**Kiambatanisho Nam. 3: Taarifa ya Wazee walio katika Mpango wa Pencheni Jamii**

| Wilaya | ME | KE | Jumla | Wapya | Waliofariki |
|---|---|---|---|---|---|
| Kaskazini "A" | 1,455 | 2,207 | 3,662 | 134 | 185 |
| Kaskazini "B" | 687 | 999 | 1,686 | 53 | 94 |
| Kati | 855 | 1,026 | 1,881 | 92 | 109 |
| Kusini | 446 | 686 | 1,132 | 49 | 74 |
| Magharibi "A" | 763 | 1,101 | 1,864 | 246 | 99 |
| Magharibi "B" | 1,077 | 1,366 | 2,443 | 384 | 95 |
| Mjini | 2,434 | 2,812 | 5,246 | 630 | 265 |
| **Jumla Unguja** | **7,717** | **10,197** | **17,7914** | **1,588** | **921** |
| Mkoani | 1,242 | 1,625 | 2,867 | 380 | 106 |
| Chakechake | 1352 | 1,727 | 3,079 | 373 | 142 |
| Wete | 1,564 | 2,242 | 3,806 | 532 | 160 |
| Micheweni | 1,121 | 1,530 | 2,651 | 271 | 77 |
| **Jumla Pemba** | **5,279** | **7,124** | **12,347** | **1,556** | **508** |
| **Jumla Kuu** | **12,996** | **17,321** | **30,317** | **3,144** | **1,429** |

**Chanzo: WMJJWW, 2023/24**

## Kiambatanisho Nam. 4: Malalamiko ya Matunzo na Mvutano wa Malezi

| **Aina ya Malalmiko/ Zanzibar** | **Yaliyoripotiwa** | | **Yaliyopatiwa ufumbuzi** | | **Yaliyopelekwa Rufaa** | | **Yanayoendelea na Usuluhishi** | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Unguja | Pemba | Unguja | Pemba | Unguja | Pemba | Unguja | Pemba |
| Matunzo | 205 | 228 | 98 | 220 | 53 | 06 | 54 | 02 |
| Mvutano wa Malezi | 108 | 150 | 58 | 132 | 23 | 18 | 27 | 00 |
| **Jumla** | **313** | **378** | **156** | **352** | **76** | **24** | **81** | **02** |

## Kiambatanisho nam. 5: Wahanga waliopo nyumba salama

| Sababu za Kupokewa Kwenye Nyumba | Jinsia | | Umri | Jumla |
|---|---|---|---|---|
| | KE | ME | | |
| Usafirishaji Haramu | 12 | 1 | 11-18 | 13 |
| Kupotea | 1 | 5 | 9-13 | 6 |
| Kupewa sumu | 1 | 0 | 1 | 1 |
| Ndoa za umri mdogo | 1 | 0 | 16 | 1 |
| Kutoroshwa | 2 | 0 | 6 - 18 | 2 |
| Kuzurura/Omba Omba | 2 | 0 | 13 -15 | 2 |
| Mvutano wa malezi | 7 | 4 | 5-19 | 11 |
| Kutelekezwa | 1 | 0 | 7 | 1 |
| Mgonjwa | 1 | 0 | 16 | 1 |
| Kupigwa | 5 | 3 | 7- 19 | 8 |
| Kutoroka | 3 | 1 | 8-17 | 4 |
| Mzazi yupo kizuizini | 2 | 0 | 1 - 2 | 2 |
| Kudhalilishwa kingono | 12 | 2 | 5- 17 | 14 |
| **Jumla kuu** | **50** | **16** | | **66** |

Chanzo: WMJJWW, 2023/24

## Kiambatanisho Nam. 6: Makosa yaliopelekea watoto kupokewa katika Kituo cha Marekebisho ya Tabia

| Aina ya Makosa | KE | ME |
|---|---|---|
| Wizi | 01 | 04 |
| Kukashifu | 0 | 02 |
| Kuondoka nyumbani | 03 | 04 |
| Kubaka | 0 | 03 |
| Kulawiti | 0 | 02 |
| Kutorosha | 0 | 04 |
| Uvutaji wa Bangi | 0 | 01 |
| **JUMLA** | **04** | **20** |

Chanzo: WMJJWW, 2023/24

## Kiambatanisho Nam. 7: Vituo Vya Kulea Watoto Yatima

| JINA LA KITUO | KE | ME | IDADI YA WATOTO |
|---|---|---|---|
| 1. Mazizini | 10 | 21 | 31 |
| 2. Fatma House | 18 | 26 | 44 |
| 3. Kidundo Orphanage Center | 10 | 15 | 25 |
| 4. S.O.S | 12 | 15 | 27 |
| 5. Darul - Ahbaab - Pemba | 00 | 43 | 43 |
| 6. Sakina Girls | 20 | 0 | 20 |
| 7. Salim Turkey Foundation | 24 | 0 | 24 |
| 8. Assalam Orphanage Center | 10 | 27 | 37 |
| 9. Zaso Children's Home | 22 | 24 | 46 |
| 10. Al- Maftuh Foundation | 35 | 18 | 53 |
| 11. Amani Foundation | 07 | 09 | 16 |
| 12. Al- Nassir Foundation | 14 | 0 | 14 |
| Jumla | **182** | **198** | **380** |

**Chanzo: WMJJWW 2024**

**Kiambatanisho Nam. 8: Vituo vya Malezi na Makuzi ya Awali ya Mtoto**

| Wilaya | Majina ya Vituo | Jumla | Idadi | | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|
| **Unguja** | | | **KE** | **ME** | |
| Mjini | Bright Mind | 13 | - | - | - |
| | Beautiful Mind Day Care and KG | | 04 | 02 | 06 |
| | Smart Kids | | 04 | 08 | 12 |
| | Step Ahead | | 06 | 04 | 10 |
| | Muqadam | | 01 | 02 | 03 |
| | London | | 10 | 13 | 23 |
| | Itaqillah | | 10 | 13 | 23 |
| | Lale Bustani | | - | - | - |
| | Iqra Integrated Academy | | | | 20 |
| | Glorious Academy | | - | - | - |
| | Dreams Light Day | | 03 | 03 | 06 |
| | Royal Children Centre | | 01 | 07 | 08 |
| | Sweet Baby Care | | 03 | 17 | 20 |
| Magharibi A | Horizon Academy | 04 | 09 | 09 | 18 |
| | Education Plus | | 06 | 06 | 12 |
| | Brilliant Academy | | 55 | 46 | 101 |
| | Al Mazraf Day Care | | 02 | 03 | 05 |
| Magharibi B | SSP | 21 | 03 | 05 | 08 |
| | High Vision | | - | - | - |
| | Kids Space | | 03 | 05 | 08 |
| | High Achievement | | 03 | 03 | 06 |
| | MJ Islamic School | | 08 | 04 | 12 |
| | Laureate International School | | 10 | 10 | 20 |
| | Al Uhudi | | 04 | 05 | 09 |
| | Feza School | | 07 | 11 | 18 |
| | First Class Academy | | 02 | 04 | 06 |
| | Al Jawaher | | 19 | 13 | 32 |
| | Kitalu Day | | 05 | 08 | 13 |
| | Zanzibar Baby Care | | 09 | 07 | 16 |
| | Milestone Day Care and KG | | 22 | 24 | 46 |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | First Step Day Care | | 06 | 10 | 16 |
| | High View School of Zanzibar | | 37 | 32 | 68 |
| | Welness Day Care Academy | | 05 | 11 | 16 |
| | Zanzibar Junior Academy | | 02 | - | 02 |
| | The Nest Day Care | | 04 | 05 | 09 |
| | Yamy Yamy Academy | | - | - | - |
| | Bright Star Day Care Centre | | 06 | 04 | 10 |
| | Alif Day Care Centre | | - | - | - |
| Kaskazini B | Amici Marafiki | 01 | 18 | 21 | 39 |
| Kati | Semta Baby Care | 01 | - | - | - |
| **Jumla** | | **40** | **287** | **315** | **621** |
| **Pemba** | | | | | |
| Wete | Maandalizi Kamaria | 4 | - | 26 | 26 |
| | Rash-Ahmed Victory | | 26 | - | - |
| | Genius Kids Nursery | | 03 | 03 | 06 |
| | Best View Nursery | | 03 | 12 | 15 |
| | Istiqama – Wete Islamic | | 05 | 10 | 15 |
| Chake chake | Maktaba Nursery | 3 | 20 | 15 | 35 |
| | Better Change | | 07 | 03 | 10 |
| | Alite Madungu Nursery | | 12 | 08 | 20 |
| Mkoani | Atlas | 3 | 06 | 09 | 15 |
| | New Mission Nursery | | 08 | 12 | 20 |
| | Mkanyageni Day Care Centre | | 15 | 08 | 23 |
| **Jumla** | | **10** | **132** | **124** | **256** |
| **JUMLA KUU** | | **50** | **419** | **439** | **877** |

**Chanzo: WMJJWW 2024**

**Kiambatanisho Nam. 9a: Watumishi waliopo masomoni kwa muda Mrefu**

| Kiwango cha Elimu | Jinsia | | Jumla | Aina ya Mafunzo |
|---|---|---|---|---|
| | Ke | Me | | |
| 1. Ufuatiliaji na Tathmini | - | 2 | 3 | Shahada ya Uzamivu |
| 2. Kiswahili | 1 | - | | |
| 2. Uchumi wa Kijamii | 1 | - | 10 | Shahada ya Uzamili |
| 3. Uchumi na Maendeleo ya Jamii | 2 | 1 | | |
| 4. Ustawi wa Jamii | 2 | 3 | | |
| 5. Ufuatiliaji na Tathmini | 1 | - | | |
| 6. Ushauri Nasaha na Saikolojia | 1 | - | 5 | Shahada ya Kwanza |
| 7. Jinsia na Maendeleo | 1 | - | | |
| 8. Rasilimali Watu na Uendeshaji | 1 | - | | |
| 9. Ustawi wa Jamii | 1 | - | | |
| 10. Uchumi | - | 1 | | |
| 11. Teknolojia ya Habari | - | 2 | 5 | Astashahada (Cheti) |
| 12. Uendeshaji wa Programu za Biashara | - | 1 | | |
| 13. Utawala wa Umma | 1 | - | | |
| 14. Utunzaji wa Kumbukumbu | 1 | - | | |
| **Jumla** | **13** | **10** | **23** | |

**Chanzo: WMJJWW, 2023/24**

**Kiambatanisho Nam. 9b: Watumishi waliopo masomoni kwa muda Mfupi**

| Aina ya Mafunzo | Jinsia | | Jumla |
|---|---|---|---|
| | Ke | Me | |
| 1. Mafunzo ya uingizaji wa taarifa za watumishi katika mfumo wa mfuko wa huduma ya afya. | 1 | 1 | 2 |
| 2. Mafunzo ya mfumo ya malipo "Pay Roll System" | 1 | 1 | 2 |
| 3. Mafunzo ya mfumo ya uwasilishaji wa michango ya watumishi "ZSSF" | 1 | 1 | 2 |
| 4. Mafunzo ya Udereva | | 2 | 2 |
| 5. Mafunzo ya vibali vya safari za nje ya nchi | | 2 | 2 |
| 6. Mafunzo ya viashiria hatarishi "Risk Management" | 3 | 2 | 5 |
| 7. Mafunzo ya ufuatiliaji tathmini ya usimamizi wa mali za umma | 1 | 1 | 2 |
| **Jumla Kuu** | **7** | **10** | **17** |

**Chanzo: WMJJWW 2024**

**Kiambatanisho Nam. 10: Idadi ya wafanyakazi kwa mujibu wa Elimu zao**

| VIWANGO VYA ELIMU | IDADI YA WAFANYAKAZI | | Jumla |
|---|---|---|---|
| | KE | ME | |
| 1. Shahada ya Uzamivu | - | 01 | **01** |
| 2. Shahada ya Uzamili | 12 | 10 | **22** |
| 3. Shahada ya Kwanza | 51 | 30 | **81** |
| 4. Diploma | 27 | 06 | **33** |
| 5. Cheti | 18 | 07 | **25** |
| 6. Kidato cha VI | 05 | 05 | **10** |
| 7. Kidato cha IV | 29 | 15 | **44** |
| 8. Chini ya Kidato cha IV | 47 | 40 | **87** |
| Jumla | **189** | **114** | **303** |

**Chanzo: WMJJWW, 2024**

**Kiambatanisho nam. 11: Watendaji wa Wizara za SMZ waliopatiwa mafunzo ya Bajeti zenye kuzingatia Usawa wa Kijinsia**

| Majina ya Wizara | Idadi ya | |
|---|---|---|
| | KE | ME |
| 1. Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda | 01 | - |
| 2. Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi | 02 | - |
| 3. Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo | 01 | 01 |
| 4. Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale | 02 | - |
| 5. Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi | 01 | 01 |
| 6. Wizara ya Maji, Nishati na Madini | - | 01 |
| 7. Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ | 01 | 01 |
| 8. Ofisi ya Makamo wa Pili | 01 | 01 |
| 9. Ofisi ya Rais Kazi, Uchumi na Uwekezaji | - | 01 |
| 10. Ofisi ya Rais Ikulu | 01 | 01 |
| Jumla | 10 | 07 |

**Chanzo: WMJJWW 2024**

**Kiambatanisho namba 12: Orodha ya vikundi vilivyotembelewa katika uhamasishaji wa uanzishaji wa Majukwaa ya Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi Unguja na Pemba mwezi wa Disemba, 2023 hadi Februari 2024**

| Mkoa | Wilaya | Shehia | Idadi ya Vikundi | Idadi ya Wanavikundi |
|---|---|---|---|---|
| MJINI MAGHARIBI | MJINI | Mwembemakumbi, Maruhubi, Msumbani, Chumbuni, Bitiamrani, Mpendae, Mchangani, Malindi, Sebleni, Amani, Chumbuni, Kwamtipura, Kwaalinatu, Mkele, Kwaalimsha, Gulioni, Meya, Magomeni, Mwembeshauri, Muembeladu, Karakana, Mboriborini, Urusi, Kilamahewa Bondeni, Kisiwanduwi, Vikokotoni, Kiponda, Rahaleo, Kwamtumwa jeni, Nyerere, Matarumbeta, Muungano na Madema. | 94 | 2,820 |
| | MAGHARIBI "A" | Mchikichini, Kizimbani, Kianga, Mtoni madukani, Welezo, Bububu Chemchem, Kibweni, Dole, Uholanzi, Kijichi, Sharifumsa, Kama, Kihinani, Mwanyanya, Mtoni Kigomeni, Regeza mwendo, Chuwini, Masingini, Mtoni Kidatu, Kwagoa na Mtoni branch. | 100 | 3,000 |
| | MAGHARIBI "B" | Kisauni, Fuonikipungani, Muembemajogoo, Mbweni, Chukwani, Mwanakwerekwe, Mnarani, Shakani , Pongwe Nyamnzi na Kombeni | 50 | 1,500 |
| KUSINI UNGUJA | KUSINI | Kitogani, Bwejuu, Dongwe, Jambiani kikadini, Muungoni, Muyuni "A", Muyuni | 33 | 990 |

| Mkoa | Wilaya | Shehia | Idadi ya Vikundi | Idadi ya Wanavikundi |
|---|---|---|---|---|
| | | "B", Muyuni "C", Kizimkazi Mkunguni, Mzuri, Pongwe na Bwejuu | | |
| | KATI | Umbuji, Dungakiembeni, Ubago Chwaka, Kikungwi, Koani, Miwani na Kidimni | 60 | 1,800 |
| KASKAZINI UNGUJA | KASKAZINI "A" | Masingini, M/shauri, Chaanikubwa Kidombo, Mkwajuni, Chutama na Kibeni. | 30 | 900 |
| | KASKAZINI "B" | Zingwezingwe, Kiomba vua, Bumbwinimisufini, Kidanzini, Mkadini, Makoba, Mafufuni, Fujoni, Mgambo | 88 | 2,640 |
| **JUMLA KUU UNGUJA** | | | **455** | **13,650** |
| KUSINI PEMBA | CHAKECHAKE | Chachani, Uwandani, Vitongoji, Mfikiwa, Chonga, Msingini, Ole, Chanjaani, Dutani, Tibirinzi, Wara, Kilindi, Tundauwa, Mchangamrima, Shungi, Uwandani, Ng'ambwa, Mtoni, Kibokoni na Ziwani. Madungu, Michungwani, Mbuzini, Wawi, Kichungwani, Ndagoni,Gombani na Masingini. | 164 | 4,920 |
| | MKOANI | Ngwachani, Kangani, Mkanyageni, Chole, Mbuguani, Tangani, Makombeni, Muyuni, Uweleni, Kengeja, Kukuu, Ngombeni, Chumbageni, Chambani, Michenzani, Makoongwe, Minazini, Kendwa, Mjimbini, Mteng'ombe, Andikoni, Mbuyuni, Mizingani, Mwambe, Mkungu, Mtambile, Jongwe, Dodo, Mchakwe, Mgagadu, Tombwe, Changawe, Kwa msharifu, Mji | 223 | 6,690 |

| Mkoa | Wilaya | Shehia | Idadi ya Vikundi | Idadi ya Wanavikundi |
|---|---|---|---|---|
| | | kunju na Ukutini. | | |
| KASKAZINI PEMBA | WETE | Junguni, Mjananza, Kiuyu minungwini, Ukunjwi, Selem, Kigongoni, Kipangani, Fundo, Mtambwekaskazini, Piki, Chwale, Utaani, Mzambarau takau, Kiungani, Limbani, Kangagani, Mtambwe Kusini, Finya, Kizimbani, Shengejuu, Kiungoni, Kinyikani, Kisiwani, Mchnga mdogo, Selem, Mlindo na Mtemani. | 155 | 4,650 |
| | MICHEWENI | Micheweni , Kinoe, Mapofu, Tumbe Mashariki, Mjini wingwi, Sizini, Mtemani, Chaleni, Shumba viamboni, Maziwa ngombe, Musuka mashariki, Msuka magharibi, Chwaka, Majenzi, Kifundi, W/Mtemani, Makangale, W/Njuguni, Kinowe, Tondooni, Shumba vyamboni, Majenzi, Mbuyuni, Tumbe magharibi, Konde na Shumba mjini. | 139 | 4,170 |
| **JUMLA KUU PEMBA** | | | **681** | **20,430** |

**Chanzo: WMJJWW 2024**

**Kiambatisho nam. 13: Malalamiko ya Wanawake yaliopokewa**

| Malalamiko | Idadi |
|---|---|
| Kunyimwa matunzo | 2 |
| Mvutano wa malezi | 3 |
| Kubaka na kuingiliwa kinyume na maumbile | 2 |
| Kupatiwa huduma ya ushauri nasaha | 2 |
| Madai ya makaazi | 1 |
| Kubakwa na ujauzito | 2 |
| Kukashifu | 1 |
| Madai ya Mahari | 1 |
| Kupigwa | 1 |
| Kutoroshwa | 1 |
| **JUMLA** | **16** |

**Chanzo: WMJJWW, 2024**

**Kiambatisho nambari 14: Idadi ya vipindi vilivyorushwa juu ya Kupinga udhalilishaji kwa wanawake na watoto**

| Kituo Cha Habari/ Gezeti | Idadi ya Vipindi | Mada zilizowasilishwa |
|---|---|---|
| 1. ZBC Redio | 11 | Udhalilishaji kwa wanawake na watoto pamoja na njia za kuondosha udhalilishaji huo katika jamii. |
| 2. Redio Assalam | 6 | |
| 3. Bahari FM | 10 | |
| 4. Redio Jamii Mtegani Kusini | 1 | |
| 5. Zanzibar Cable Televisheni | 8 | |
| 6. ZBC TV | 4 | |
| 7. Zanzibar Leo | 10 | |
| Jumla ya vipindi | **50** | |

**Chanzo: WMJJWW, 2024**

## Kiambatanisho nam. 15: Mgawanyo wa fedha kwa mwaka wa fedha 2024/2025

| Fungu / Programu | Kazi za Kawaida '000 | | | | Kazi Za Maendeleo '000 | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Jumla Kuu | Mishahara | Matumizi ya Kawaida Smz | Matumizi ya Kawaida UNICEF/ GEF | Smz | Wahisani | | | Jumla |
| | | | | | | UN WOMEN | UNFPA | WB | |
| PH0401 Hifadhi ya Jamii | 5,789,835 | - | 1,105,335 | 193,500 | 4,500,000 | - | - | - | 4,500,000 |
| PH0402 Utawala na Uendeshaji | 15,133,514 | - | - | - | - | - | - | - | - |
| SH040201 Utawala na uendeshaji | 4,738,047 | 3,321,006 | 1,417,042 | - | - | - | - | - | - |
| SH04202 Mipango Sera Na Utafiti | 8,992,763 | | 401,552 | 479,586 | - | - | - | 8,111,626 | 8,111,626 |
| SH040203 Utawala na Uendeshaji Ofisi kuu Pemba | 1,402,704 | 573,994 | 828,710 | - | - | - | - | - | - |
| PH0403 Maendeleo ya Jamii na Jinsia | 2,392,112 | - | 631,562 | 1,016,550 | - | 536,000 | 208,000 | - | 744,000 |
| **JUMLA** | **23,315,461** | **3,895,000** | **4,384,201** | **1,689,636** | **4,500,000** | **536,000** | **208,000** | **8,111,626** | **13,355,626** |

**Chanzo: WMJJWW 2024**